



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NZEGA**



Unapojibu tafadhali taja

Kumb.Na. NTC/CA4/2/80

TAREHE 24/08/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nzega amepokea Kibali cha Ajira Mbadala chenye **Kumb.Na FA.170/365/01/"B"/130** cha tarehe **22 Julai, 2021** kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**. Katika Nafasi zifuatazo:

- 1. Mtendaji wa Mtaa Daraja la III – Nafasi 01**
- 2. Dereva Daraja la II - Nafasi 01**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nzega anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo kama ilivyo ainishwa katika Tangazo.

MTENDAJI WA MTAA III - TGS B (NAFASI 01).

1.0 MTENDAJI WA MTAA DARAJA LA III – (NAFASI 01)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (IV) au Kidato cha sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya cheti/Astahada (**Cheti cha NTA LEVEL 5**) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

